

# **Tungo za Kinahau Zinazotoa Taarifa ya Mpira wa Miguu katika Magazeti ya Kiswahili**

*Sabra Ahmed*

## **Ikisiri**

Makala haya yanachambua tungo za kinahau zinazotoa taarifa ya mpira wa miguu katika magazeti ya Kiswahili nchini Tanzania. Kazi hii inajikita kuchambua maana mbalimbali za kimazingira zinazotokana na tungo za kinahau zinazotumiwa na waandishi wa magazeti katika kutoa taarifa za mpira wa miguu. Makala pia yanabainisha vigezo ambavyo waandishi hutumia katika kuchagua tungo za kinahau kutoa taarifa zao. Halikadhalika, makala yanabainisha wazi sababu zinazopelekea waandishi wa ripoti za mpira wa miguu kutumia tungo hizo za kinahau. Mbali na hayo, data za makala haya zimepatikana kwa njia ya kusoma magazeti ya michezo pamoja na kusaili waandishi 40 wa magazeti ya michezo. Magazeti yaliyotumiwa na makala haya ni *Bingwa, Lete Raha, Spoti Starehe, Burudani, Mwana Spoti* na *Dimba*. Mwandishi ameteua magazeti haya ili kuweza kupata data halisi kuhusiana na tungo za kinahau zinazotumiwa na waandishi kutoa taarifa za mpira wa miguu. Pia, mwandishi wa makala haya ameteua taarifa za mpira wa miguu kwa sababu waandishi wa taarifa hizi hutumia kwa kiasi kikubwa tungo za kinahau ili kuvuta wasomaji wao pamoja na kuuza magazeti yao. Utafiti huu ulitumia data zilizokusanywa mwaka 2009. Msingi unaoongoza makala haya ni kuwa lugha hupata maana kulingana na mazingira inamotumika.

## **1.0 Utangulizi**

Wataalamu wafuatao wamejaribu kuelezea dhana ya nahau: TUKI (2004) inaeleza kuwa nahau ni fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana ya kawaida. Fasili hiyo inaungwa mkono na waandishi wengine kama Gibbs (2002) na Nippold na Duthie (2003). Hivyo basi, makala haya yamechambua tungo za kinahau kwenye magazeti ya michezo kwa kufuatana na fasili iliyotolewa hapo juu. Lugha ya michezo huwa ni tofauti na lugha zinazotoa taarifa nyingine katika magazeti. Waandishi kwa kawaida huandika kwa lugha ambayo itawavutia wasomaji wake. Hivyo, huchagua maneno ambayo yanaweza yakaleta mvuto katika taarifa zao. Kwa mujibu wa Mensah (1995) waandishi wa habari za mpira katika magazeti hutumia lugha ambayo si rasmi, hivyo wanakiuka sheria za uandishi. Utafiti wetu unaona kuwa mtazamo wa Mensah umeshindwa kugundua kuwa kila taarifa katika magazeti huwa ina mtindo wake wa uwasilishaji taarifa hizo. Hivyo, lugha inayotumika kuripoti taarifa za michezo ni tofauti na ile inayowasilisha taarifa za kisiasa au kiuchumi (taz. Halliday, 1978; Crystal, 1995; Fowler, 1996). Michezo ni burudani, kila mtu anatarajia anaposoma taarifa hizo kwenye magazeti aipate burudani hiyo.

Makala haya yataongozwa na nadharia yenye mwelekeo wa kipragmatiki. Yaani, lugha hupata maana kulingana na mazingira inamotumika (Halliday na Hassan, 1985; Yule, 1996 na Langacker, 2001). Nadharia hii imesaidia katika kuchambua maana ya tungo za kinahau zilizotumiwa katika kuwasilisha taarifa za mpira wa miguu katika magazeti. Moore (2001) anafafanua kwamba lugha ya kuwasilisha taarifa ya mpira wa

miguu huwezi kuitafsiri neno kwa neno au kirai kwa kirai lazima uhusianishe na muktadha uliotumika ndipo utapata maana. Yule (1996) anaongezea kwa kusema kwamba mwandishi/mzungumzaji huwa na maana kinyume na maana ya kawaida ya maneno anayoandika au anayozungumza. Yaani, msemaji huandika au huzungumza sentensi ambayo maana yake ni tofauti na maneno yaliyotumiwa katika sentensi ama tungo hiyo. Kwa mfano, '*Simba yairarua Yanga*' maana ya sentensi hii ni kwamba timu ya mpira wa miguu iitwayo Simba imeifunga timu ya Yanga. Lakini neno '*yairarua*' kwa maana ya kawaida ni kuchanachana na siyo kufunga.

## **2.0 Tungo za Kinahau kuhusu Mpira wa Miguu Magazetini**

Mchezo wowote ive mpira wa miguu au michezo mingine matokeo huwa ni kushinda au kushindwa. Waandishi wa magazeti ya michezo huwa wanatumia tungo za kinahau tofauti tofauti kuashiria timu imeshinda au imeshindwa. Sehemu inayofuata inafafanua tungo za kinahau kutoka kwenye magazeti ya michezo na maana zake kulingana na mazingira ya mpira wa miguu. Mwandishi wa makala haya amezigawanya tungo hizi katika makundi kulingana na maana zake.

### **2.1 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Timu Iliyoshinda**

Waandishi wa taarifa hizi za mpira wa miguu katika magazeti yao wanatumia tungo tofauti za kinahau kumaanisha kwamba timu imeshinda. Baadhi ya tungo hizo ni:

*Andika bao*  
*Bwaga bao 1 - 0*  
*Fyeka kwa mabao 3 - 1*  
*Gagadua mabao 2 - 0*  
*Rarua mabao 3-0*  
*Lamba mabao 2 -0*  
*Nyoo kwa bao 1 - 0*  
*Sulubu kwa mabao 3 -0*  
*Tandika mabao 3 -0*

Mtu akichunguza maneno haya: *andika, bwaga, fyeka, gagadua, lamba, nyoo, sulubu* na *tandika* atapata maana kuwa ni 'funga au shinda' katika mazingira ya mpira wa miguu. Lakini maneno haya katika matumizi ya kawaida yana maana tofauti kabisa. Mwandishi hutumia maneno haya kuonesha kwamba mpira wa miguu ni kama vita kati ya timu mbili zinazokinzana. Ndiyo maana wanatumia maneno ya ubabe au vitisho kama *tandika, rarua, sulubu, fyeka, bwaga* na *gagadua*. Wakati mwingine, waandishi hutumia maneno *lamba* au *nyoo* kuonesha timu imeshinda kwa kuwa kushinda huku ni sawa na kuondoa uchafu au kujisafisha. Hivyo basi, waandishi wa mpira wa miguu huchagua maneno ya kinahau kulingana na dhumuni au jambo analotaka kuliwasilisha kwa wasomaji wao. Hii inathibitika kutoka kwa wanapragmatiki kama (Halliday, 1978; Crystal, 1995 na Fowler, 1996) kwamba lugha inatofautiana kulingana na jambo linalozungumziwa. Sasa hebu tuangalie upande wa pili wa shilingi.

## 2.2 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Timu Iliyoshindwa

Waandishi wa magazeti ya michezo hutumia tungo mbalimbali za kinahau kuonesha timu fulani imeshindwa mechi. Chunguza tungo zifuatazo:

*A.F.C ilikuwa dabwadabwa kwa Simba  
Cheki nayo kimeo  
Lala kwa mabao 2 - 0  
Liverpool yalimwa mabao 2 -0  
Yanga ilikuwa rojorojo kwa Simba*

Ukizichunguza tungo za hapo juu utapata maana kwamba timu fulani imeshindwa mechi. Maneno *dabwadabwa*, *kimeo*, *lala*, *limwa* na *rojorojo* yametumika kinahau kuonesha kushindwa kwa mechi au timu imeshindwa kuonesha uwezo wake na kushindwa mechi hiyo. Lakini katika mazingira ya kawaida ambayo ni tofauti na mazingira ya mpira wa miguu tungo za hapo juu hazitakuwa na maana yoyote. Moore (2001) anathibitisha hilo kwa kusema kuwa lugha ya mpira wa miguu ukitafsiri neno kwa neno hutaweza kupata maana iliyokusudiwa. Aidha, waandishi wa ripoti za mpira wa miguu hutumia tungo za kinahau kuashiria matangazo ya mechi. Sehemu ifuatayo inafafanua hilo.

## 2.3 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Matangazo ya Mechi

Waandishi wa mpira wa miguu pia hutumia tungo za kinahau kutoa matangazo ya mechi kuwa timu fulani zitacheza leo usiku au kesho au wiki ijayo. Hebu tuchunguze tungo zifuatazo:

*Timu zitakumbana kesho  
Timu zitakwaana leo usiku  
Timu zitapepetana kesho  
Timu zitaumana siku ya Jumapili  
Timu zitavaana usiku wa leo*

Katika mazingira ya mpira wa miguu, tungo za hapo juu zinatoa maana kuwa timu hizo mbili zitacheza mpira wa miguu kesho, leo usiku, Jumapili na kadhalika. Waandishi wanatumia maneno ya kinahau kama *kumbana*, *kwaana*, *pepetana*, *umana* na *vaana* ili kuonesha kwamba mechi ni sawa na vita au ngumi na lazima zioneshane ubabe ili mmoja aibuke mshindi. Vilevile, ukichunguza vitenzi hivyo vya kinahau huwa vinatumia viambishi vya kutendana 'an' ili kuonesha kuwa hilo pambano ni la wawili (Shadeberg, 2003). Mbali na tungo zinazoashiria matangazo ya mechi, sehemu inayofuata inafafanua tungo za kinahau ziashiriazao sifa ya mchezaji au timu.

## 2.4 Tungo za Kinahau Ziashiriazio Sifa ya Mchezaji au Timu

Waandishi wa mpira wa miguu hutumia tungo za kinahau zifuatazo kuonesha sifa ya timu fulani au sifa ya mchezaji fulani:

*Timu ina wembe mkali*  
*Timu /mchezaji ni kifaa*  
*Mchezaji fulani atema cheche zake*  
*Mchezaji fulani ni moto wa kuotea mbali*

Maneno kama *wembe*, *kifaa*, *cheche* na *moto* hutumika kinahau kuonesha kuwa timu fulani ni nzuri kwa kuwa na mchezaji au wachezaji wazuri wenye ujuzi kisoka. Nomino *moto*, *cheche*, na *wembe* ni vitu ambavyo vinaogopwa na binadamu, hivyo waandishi huzitumia kinahau katika tungo zao ili kuonesha kwamba mchezaji huyo anaogopwa na wachezaji pinzani kutokana na ujuzi wake wa kucheza mpira wa miguu au timu hiyo inaogopwa na timu pinzani kwa kuwa na wachezaji wazuri. Hivyo, maana ya kinahau katika tungo hizo zina uhusiano na maana za msingi za maneno hayo kama inavyohibitika kwa Gibbs (2002) kuwa maana ya tungo za kinahau zina uhusiano na maana za msingi au kawaida za tungo hizo. Vilevile, Gibbs (kata) anaongezea kwa kusema kuwa sio tungo zote za kinahau ambazo huweza kupata maana kutokana kuhusianisha na maana za msingi. Kwa mfano, neno '*kifaa*' limezuka katika jamii yetu ya Kitanzania kumaanisha kitu kizuri/mtu mzuri au mwenye akili ama mchapa kazi. Kwa mfano, '*Yule ni kifaa*' ina maana kuwa yule ni mzuri au mwenye akili ama mchapa kazi. Maana hii ni tofauti na maana ya msingi ya neno kifaa. Hivyo, waandishi wa mpira wa miguu wameweza kuhamisha maana hii ya kinahau katika taarifa zao kuonesha kuwa mchezaji ni mzuri kimchezo au anatumia akili katika uchezaji wake ama anajituma uwanjani. Hata hivyo, zipo tungo za kinahau ambazo hutumiwa na waandishi wa mpira wa miguu katika ripoti zao zinazoashiria timu imepata pointi. Sehemu ifuatayo hufafanua tungo hizo.

## 2.5 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Timu Imepata Pointi

Waandishi wa mpira wa miguu hutumia tungo za kinahau zifuatazo kuonesha timu kuwa imepata pointi katika mechi au shindano:

*Zoa pointi*  
*Nyakua pointi*  
*Chota pointi*

Waandishi hutumia maneno *zoa*, *nyakua* na *chota* kuonesha kwamba ushindi uliopatikana sio wa kawaida bali ni wa nguvu au timu iliyoshindwa ilikuwa imezidiwa kwa kiasi kikubwa na timu iliyoshindana nayo. Hivyo, maana za msingi za maneno hayo ni tofauti na maana hizo za kimazingira au kinahau hivyo ni vigumu kwa mtu ambaye si mzawa au mjuzi wa lugha hiyo kupata maana ilyokusudiwa (Nippold na Duthie 2003 na Nicholls 2003). Sehemu inayofuata inafafanua tungo za kinahau zinazoashiria timu imemaliza mchezo bila kufungana.

**2.6 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Timu Imemaliza Mchezo bila Kufungana**  
 Waandishi wa ripoti za mpira wa miguu hutumia tungo za kinahau zifuatazo kuashiria timu imemaliza mchezo wake bila kufungana magoli:

*Walitoka nunge  
 Bila majibu*

Wakati mwingine tungo '*bila majibu*' huweza kumaanisha timu pinzani imeshindwa kurudisha (ma)goli aliyofungwa na timu inayocheza nayo. Hivyo basi, tungo za kinahau zinaweza kuwa na maana zaidi ya moja kulingana na matumizi na jinsi zilivyotumika. Mbali na hayo, zipo tungo za kinahau ambazo waandishi hutumia kuashiria kutoa pasi kwa mchezaji. Sehemu inayofuata inafafanua.

**2.7 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Kutoa Pasi kwa Mchezaji**

Waandishi wanaoandika ripoti za mpira wa miguu katika magazeti hutumia tungo za kinahau kama '*penyeza pasi*', *kuonana* na '*megea pande*' kumaanisha kumpasia mpira mchezaji mwenzake wa timu moja. Kwa mfano, '*Nico Nyagawa alimpenyezea pasi Mgosi*'. Katika mazingira ya mpira wa miguu tungo hii inamaanisha kuwa Nico Nyagawa alimpasia mpira Mgosi ambaye ni mchezaji mwenzake wa timu ya Simba. Hivyo maneno *penyeza*, *onana* na *megea pande* hutumika kinahau katika taarifa za mpira wa miguu ili kuleta msisimuko kwa wasomaji wao. Aidha, waandishi wa ripoti za mpira wa miguu hutumia tungo za kinahau zinazoashiria timu ni imara kama inavyofafanuliwa katika sehemu inayofuata

**2.8 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Timu ni Imara**

Waandishi vilevile hutumia maneno ya kinahau katika taarifa zao kama '*majogoo*', '*vidume*', '*wababe*' na '*miamba*' kumaanisha timu hizo ni imara. Kwa mfano, '*majogoo wawili watachuana kesho*'; '*wababe wawili wataoneshana ubabe wao leo usiku*' na '*miamba miwili itakutana kesho*'. Tungo hizi zina maana kwamba timu hizo mbili ni imara zitachuana kesho au leo usiku. Katika sehemu inayofuata tungo za kinahau zinazoashiria shindano au mechi zimefafauliwa.

**2.9 Tungo za Kinahau Zinazoashiria Shindano au Mechi**

Waandishi pia hutumia maneno kama '*kinyang'anyiro*', '*mchuano*' na '*pambano*' kuashiria mechi ama shindano katika mazingira ya mpira wa miguu. Maneno hayo hutumika kama picha kuonesha kwamba mchezo wa mpira wa miguu ni kama vita. Musau (nk: 495) anasema mchezo ni kama pambano la kumwaga damu au vita vya kufa na kupona kati ya maadui wawili. Hii ina maana kwamba katika mchezo hakuna urafiki. Kila mtu anashindana ili aibuke mshindi. Hivyo ndiyo maana waandishi hutumia maneno hayo ya vitisho. Ingawa kuna mechi za kirafiki hata hivyo zote zinazingatia ushindani. Sehemu inayofuata inajadili tungo nyinginezo za kinahau zitumikazo katika taarifa za mpira wa miguu.

## 2.10 Tungo Nyinginezo za Kinahau Zinazotumika katika Taarifa za Mpira wa Miguu

Mbali na tungo za kinahau zilizotangulia kujadiliwa, mwandishi wa makala haya ameziweka tungo zifuatazo za kinahau zinazotumiwa na waandishi wa ripoti za mpira wa miguu na maana mbalimbali. Tungo hizi zimewekwa pamoja kwa sababu tungo za kinahau ni nyingi na zikijadiliwa kila moja peke yake itapelekea kazi hii kuwa na vipengele vingi na kusababisha kazi kuwa kubwa na kuwachosha wasomaji:

<i>Mlinda mlango</i>	goli kipa
<i>Kiungo</i>	Mchezaji wa kati anayecunganisha timu katika kupokea mpira na kutoa pasi kwa wachezaji wenzake
<i>Langoni</i>	golini
<i>Mtambaa wa panya</i>	chuma cha juu ya goli
<i>Piga bunduki</i>	piga mpira kwa nguvu
<i>Ametumia chakula</i>	ametumia nguvu
<i>Amerusha fyongo</i>	amerusha mpira bila kufuata sheria
<i>Ameza timu</i>	amekosa goli ama amefungwa kizembe
<i>Kuchechemea</i>	timu ya mwisho au imeshindwa kufanya vizuri
<i>Kung'ara</i>	timu imeshinda au imejichukulia kombe

Maana zilizowekwa mbele ya tungo za kinahau za hapo juu ni maana zinazopatikana katika mazingira ya mpira wa miguu. Maana hizo ni tofauti na maneno yaliyotumiwa katika tungo hizo. Kama alivyosema Nicholls (2003) kuwa tungo za kinahau huwezi kutafsiri neno kwa neno kwa kutumia lugha nyingine. Kwa mfano, tungo za kinahau kama '*ameza timu*' (he has sold a team) na '*ametumia chakula*' (he has used a food) ukitasfiri neno kwa neno kwa lugha ya Kiingereza huwezi kupata maana iliyokusudiwa kuwa amekosa goli ama amekosa goli kizembe na ametumia nguvu kumsukuma mwenziwe kwenye mechi na kusababisha 'faulo' au madhambi. Hivyo, waandishi wa mpira wa miguu hutumia maneno hayo kinahau ili kuvutia kazi zao ziweze kusomwa. Sehemu inayofuata inabainisha wazi kuwa waandishi wa habari za mpira wa miguu hawatumii tungo hizo za kinahau kiholela bali wana vigezo maalumu wanavyovifuata kuchagua tungo hizo katika taarifa zao.

## 3.0 Vigezo Vinavyotumiwa na Waandishi wa Mpira wa Miguu katika Uchaguzi wa Maneno ya Kinahau kwenya Taarifa zao

Waandishi wa magazeti ya michezo huwa hawatumii tungo za kinahau kiholela bali huchagua tungo hizo kwa kutumia vigezo maalumu. Kigezo cha kwanza ambacho waandishi hukutumia katika kuchagua tungo hizo za kinahau ni idadi ya magoli ambayo timu imeshinda. Kwa mfano, neno '*ua*' au '*mauaji*' kwa kawaida hutumika wakati timu imefunga magoli 3 au zaidi. Kwa kuwa tendo la kuua si kitendo cha

kawaida kwa upande wa binadamu, basi waandishi wa mpira wa miguu hutumia neno hilo kwenye taarifa zao ili kuonesha kuwa kitendo cha timu kufunga mabao zaidi ya 3 si kitendo cha kawaida kwenye mpira wa miguu. Chunguza mifano ifuatayo:

*A.F.C ilifanya mauaji ya kutisha kwa kuichabanga Mtibwa sugar 5-1. (Spotistarehe, Alhamisi, June 8-10, 2006).*

*Yanga yafanya mauaji kwa kuifunga 4-1 Bandari. (Spotistarehe, Jumapili, June 4-7, 2006).*

Mifano yote ya hapo juu inaonesha kwamba neno *mauaji* linatumika wakati timu ikiwa imefunga timu pinzani zaidi ya magoli matatu. Ni jambo la kushangaza ikiwa timu imefunga goli moja halafu mwandishi atumie neno hilo la kinahau.

Halikadhalika, umaarufu wa timu ni kigezo kinachofuata kuchagua tungo za kinahau katika kuwasilisha taarifa za mpira wa miguu. Kwa mfano, Yanga na Simba ni timu kubwa na maarufu nchini Tanzania. Moja ya timu hizi ikicheza mechi na timu ndogo kama Moro United au Prisons au A.F.C. halafu mwisho wa mchezo Yanga au Simba ikashindwa basi waandishi huchagua neno kali au maneno ya istihizai kutoa taarifa zao za michezo. Kwa mfano, maneno kama *nyolewa, tandikwa, bosholewa* na *chapwa*. Tuchunguze mifano ifuatayo:

*Yanga yachapwa bao 1-0 (Bingwa, Jumanne, Juni 13, 2006).*

*Simba yabosholewa bao 1-0 na Prisons (Majira, Jumatatu, Juni 12, 2006).*

Mifano hiyo inaonesha kwamba maneno *yachapwa* na *yabosholewa* ni makali. Hivyo si sahihi kutumia kama timu imeshindwa kwa kufungwa goli moja tu ni vyema yakatumiwa kama timu imefungwa magoli zaidi ya moja. Hata hivyo, kutumiwa kwake kwenye tungo za hapo juu kumetokana na kigezo cha umaarufu wa timu hizo na kushindwa kwake katika mchezo husika.

Kigezo kingine ni hali ya mchezo wenyewe. Kigezo hiki humsababisha mwandishi aweze kuchagua tungo za kinahau katika ripoti yake ya mpira wa miguu. Kwa mfano, kama timu fulani ilikuwa inatarajiwa kucheza vizuri kwenye mechi fulani halafu mwisho wa mchezo ikashindwa kwa kucheza vibaya. Hivyo, waandishi huchagua maneno ya kinahau kuelezea timu imeshindwa. Kwa mfano, neno *laza* linaweza kutumika. Kwa mfano, *A.F.C. Jumapili iliyopita iliwalaza wana Jangwani (Yanga) bao 1-0 (Lete Raha, Jumapili, Juni 18-24, 2006).*

Hapa mwandishi ametumia neno '*laza*' katika tungo hiyo kwa sababu Yanga ni timu kubwa Tanzania na ilitegemewa kucheza vizuri na kuishinda A.F.C ambayo ni timu ndogo. Lakini mchezo uliochezwa ulikuwa kinyume na matarajio. Hivyo, waandishi huchagua neno '*laza*' kuonesha kwamba Yanga ilikuwa imezembea au imelala.

Sehemu au mahali timu zinapochezea mechi zao ni kigezo kingine ambacho waandishi hutumia kuchagua maneno yao ya kinahau katika ripoti zao. Kwa mfano, timu fulani inachezea mechi yake kwenye uwanja wa nyumbani kwao na kisha ikafungwa mechi hiyo, basi waandishi wa ripoti za mpira wa miguu huchagua maneno makali kuonesha timu hiyo imeshindwa katika uwanja wake wa nyumbani. Kwa mfano, maneno kama *bobota*, *sulubu* na kadhalika huweza kutumika.

Hali kadhalika, waandishi huchagua maneno ya kinahau kulingana na majina ya timu za mpira wa miguu yenyewe. Kwa mfano, *Simba yairarua Yanga kwa bao 1-0*; *Mtibwa sugar yalambwa na Yanga* na *Mtibwa yaibomoa Bandari*. Ukichunguza tungo hizo utagundua kuwa neno *raru* limechaguliwa kutokana na jina la timu (Simba) ambalo linafananishwa na simba mnyama. Vilevile, neno *lambwa* limechaguliwa kutokana na jina la timu hiyo kwa sababu timu ya Mtibwa inamilikiwa na kiwanda cha sukari. Hivyo, sukari inafaa kulambwa. Pia, neno *bomoa* limeweza kutumika kutokana na kwamba timu ya Bandari inamilikiwa na mamlaka ya Bandari. Hivyo miundombinu ya bandari inaweza kubomolewa.

Mwisho kabisa, waandishi wanaweza kubadilishabadilisha maneno ya kinahau katika ripoti zao za mpira wa miguu kwa kuogopa kurudiarudia maneno ambapo kutapelekea taarifa zao za mpira kuwa chapwa. Kwa mfano, kama ripoti ya kwanza imetumia neno *chapa* au *tandika* basi, waandishi huhakikisha katika ripoti inayofuata atumie maneno mengine ya kinahau ili kuepuka kurudiarudia maneno katika taarifa zao. Kipengele kinachofuata kinaelezea sababu zinazowapelekea waandishi wa mpira wa miguu kutumia tungo za kinahau katika taarifa zao.

#### **4.0 Sababu za Kutumia Tungo za Kinahau katika Ripoti za Michezo**

Kuna sababu kadhaa ambazo huwafanya waandishi wa mpira wa miguu waweze kutumia tungo za kinahau katika taarifa zao. Katika makala haya zitajadiliwa sababu kuu nne (4). Sababu ya kwanza ni kwa ajili ya kuwaburudisha wasomaji wao. Kwa mfano, inaonekana kwamba wasomaji wa ripoti za mpira wa miguu huburudika wakisoma tungo kama: '*Simba yairarua Yanga kwa bao 2-0*' kulikoni wakisema '*Simba yaifunga Yanga kwa bao 2-0*'. Hivyo neno '*raru*' linafananishwa na simba mnyama. Kwa hiyo, neno hilo huleta burudani katika tungo hiyo kuliko kutumia neno shinda au funga ambalo ni neno la kawaida.

Pili, waandishi wa ripoti za mpira wa miguu hutumia tungo za kinahau kwa ajili ya kuvutia wateja wao (wasomaji wa magazeti) ili kuuza magazeti yao. Hivi sasa kuna makampuni mengi ya magazeti, hivyo hupelekea kuwa na ushindani wa kuuza magazeti. Hivyo, waandishi hutumia maneno mbalimbali ya kinahau kuwavutia wateja wao ili waweze kununua magazeti yao.

Ubunifu na uvumbuzi ni sababu nyingine kuu ambayo waandishi huitumia. Waandishi wanatumia tungo za kinahau katika ripoti zao ili kubuni mtindo maalumu



wa lugha ya mpira wa miguu. Mwandishi yeyote yule huruhusiwa kucheza na maneno katika uandishi wake ilimradi asivunje sheria za uandishi kwa kutumia maneno mabaya au ya matusi. Hivyo, waandishi hawa hutumia maneno haya ya kinahau kwa ajili ya kutofautisha lugha ya michezo na lugha nyinginezo (lugha ya hospitalini, sokoni, kanisani au ya kishairi).

Sababu nyingine ni kuongeza msamiati na maana mpya katika lugha ya Kiswahili. Waandishi wa taarifa za mpira wa miguu pia hutumia maneno ya kinahau ili kuingiza maana mpya na maneno mapya katika lugha ya Kiswahili na hivyo kukiendeleza na kukikuziwa Kiswahili. Kwa mfano, maneno *mwamba*, *lango*, *dimba* n.k yaimengizwa kwenye kamusi ya Kiswahili yakiwa yamepata maana mpya.

Mwisho, waandishi wa ripoti za mpira wa miguu hutumia maneno ya kinahau mara kwa mara katika taarifa zao ili kuenda na wakati. Kwa mfano, tungo kama *Cheki nayo ni kimeo*, *Simba yafunika bovu*, *Yanga yaibuka kidedea*, ni tungo zenye maneno ya Kiswahili yanayotokana na misemo (misimu) ya wakati huu.

### 5.0 Hitimisho

Makala haya yamebainisha wazi kuwa tungo zinazotumiwa kwenye ripoti za mpira wa miguu magazetini hutoa maana za kimazingira ambazo ni tofauti na maana ya kawaida. Kwa mfano, *bobota mabao*, *andika mabao*, *raru mabao*, na *laza kwa mabao* katika mazingira ya mpira wa miguu humaanisha 'funga mabao'. Lakini maneno hayo, yaani *bobota*, *andika*, *raru*, *laza* hayana maana hiyo katika mazingira ya kawaida. Pia, mwandishi wa makala haya ameweka wazi kwamba waandishi wa ripoti za mpira wa miguu hawatumii maneno yao kiholela bila kuwa na vigezo vya utuzi wa maneno hayo. Hivyo waandishi hao wana vigezo maalumu ambavyo vinawaongoza katika uchaguzi wa tungo hizo za kinahau ili kuzitumia katika taarifa zao za mpira wa miguu. Halikadhalika, waandishi wanaotoa ripoti za mpira wa miguu magazetini nchini Tanzania hutumia tungo za kinahau nyingi ili kuwavutia na kuwaburudisha wasomaji wao na kuuza magazeti yao. Vilevile, husaidia kuongeza misamiati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili na kupanua maana za maneno katika lugha hiyo. Hivyo, husaidia katika kukikuziwa na kukiendeleza Kiswahili. Mbali ya hayo, hufanya hivi kwa ajili ya kutaka kujiundia mtindo wao wa lugha wa kutoa taarifa za mpira wa miguu hapa nchini Tanzania ili kuleta upekee wa lugha yao.

**Marejeo**

- Crystal, D & D. Davy (1969). *English Language Series: Investigating English Style*. London and Harlow: Longman
- Crystal, D. (1995). *The Cambridge Encyclopaedia of the English Language*, Cambridge: Cambridge University Press
- Gibbs, R.W. (2002). "A New look at Literal Meaning in Understanding what is said and Implicated", *Journal of Pragmatics*. 34, [www.elsevier.com/locate/pragma](http://www.elsevier.com/locate/pragma) retrieved on March, 24th, 2007
- Fowler, R. (1996). *Linguistic Criticism* (2<sup>nd</sup> ed), Oxford, Oxford University Press.
- Halliday, M.A.K. (1978). *Language as Social Semiotic, The social Interpretation and Meaning*, London, Arnold
- Halliday, M.A.K. & Hassan, R. (1985). *Language, Context and Text: Aspects of Language in a Social Semiotic Perspective*, Oxford, Oxford University Press
- TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, Kenya
- Langacker, Ronald, W. (2001b). *Discourse in Cognitive Grammar*, in *Cognitive Linguistics* 12-2: 143-188
- Mensah, J.K. (1995). "Swahili Journalistic Language, a Linguistics Study (view)", <http://www.njas.helsinki.fi/ledf-files/vo/vo14num2/mensah.pdf>. Retrieved on Saturday, January 13<sup>th</sup>, 2007
- Moore, A. (2001). *How Pragmatics Works in Football Language*, <http://www.universalteacher.org.uk/lang/pragmatics.htm>. Retrieved on November 19th, 2006
- Musau, P.M. (n.k). "The Evolution and Development of Swahili Styles: The case of Football Language". In *Mehr als nur Worte, Africanistische Beiträge zum 65. Geburtstag Von Franz Rottland* (pp483-503)
- Nicholls, D. (2003). *A tough Nut to Crack Figures of Speech and the Language Learners*, <http://www.macmillandictionary.com/medmagazine/November2003/13feature-figures-of-speech.htm> retrieved on Thursday, June 15<sup>th</sup>, 2006
- Nippold, M.A. & J.K. Duthie (2003). "Mental Imagery and Idiom Comprehension: A Comparison of School – Age Children and Adults", In *Journal of Speech, Language and Hearing Research*, (Vol. 46, pp788-799), American Speech – Language – Hearing Association
- Yule, G. (1996). *Pragmatics*, Newyork: Oxford University Press